***SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR***

-------------------------------------------------------

**TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

# RIPOTI
# YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA TUME YA MAADILI KWA MWAKA 2016/2017

copy

**Septemba, 2017**

(Imewasilishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 29 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya 2015)

# YALIYOMO


YALIYOMO ..... 1

1.0 UTANGULIZI ..... 3

2.0 HISTORIA FUPI YA TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA ..... 5

2.1 DIRA ..... 6

2.2 DHAMIRA ..... 6

2.3 MAADILI YA MSINGI ..... 6

2.4 LENGO KUU ..... 7

2.5 MUUNDO WA TUME ..... 7

2.6 MAJUKUMU YA TUME ..... 8

2.7 MAMLAKA NA UWEZO WA TUME ..... 9

3.0 KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2016/17 ..... 10

4.0 UTEKELEZAJI HALISI WA KAZI ZA TUME KWA MWAKA 2016/2017 ..... 11

4.1 UANZISHAJI WA OFISI ..... 11

4.1.1 Ofisi ya Tume ..... 11

4.1.2 Upatikanaji wa Samani na Vitendea kazi ..... 12

4.1.3 Kuwajengea Uwezo Watumishi wa Tume ..... 12

4.1.4 Muundo wa Kitaasisi wa Tume ..... 13

4.2 KUPOKEA, KUSAJILI NA KUHAKIKI TAARIFA ZA MALI NA MADENI ZA VIONGOZI WA UMMA ..... 13

4.2.1 Kupokea na Kuhifadhi Tamko la Mali na Madeni kwa Viongozi wa Umma ..... 14

4.2.2 Kuhakiki Taarifa za Mali na Madeni za Viongozi wa Umma ..... 16

4.3 KUTAYARISHA MFUMO WA NDANI WA KIELEKTRONIKI WA USAJILI WA TAARIFA ZA MALI NA MADENI ..... 17

4.4 KUPOKEA NA KUFANYA UCHUNGUZI WA TUHUMA NA MALALAMIKO YA UKIUKAJI WA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA ..... 18

4.4.1 Tuhuma na Malalamiko ..... 18

4.4.2 Uvunjaji wa Maadili ..... 19

4.5 KUTOA ELIMU KWA UMMA NA VIONGOZI KUHUSU UMUHIMU WA MAADILI ..... 20

4. 5.1 Mikutano ya Viongozi wa Umma ..... 21

4.5.2 Utayarishaji na Urushaji wa Vipindi vya Elimu na Matangazo kupitia Vyombo vya Habari ..... 21


copy

4.5.3 Utoaji wa Vipeperushi, Machapisho na Matangazo........22
4.5.4 Tovuti ya Tume........23
4.5.5 Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binaadamu........23
4.6 KUTAYARISHA KANUNI ZA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA........24
5.0 VIKAO VYA TUME........24
6.0 HALI YA UPATIKANAJI WA FEDHA........25
7.0 CHANGAMOTO NA UTATUZI WAKE........25
8.0 MIKAKATI YA TUME KWA MWAKA 2017/2018........26
9.0 MAPENDEKEZO........27
10.0 HITIMISHO........27
11.0 UWASILISHAJI WA RIPOTI........29

copy

## 1.0 UTANGULIZI

Maadili ni dhana pana inayomgusa kila mtu katika maisha yake ya kila siku. Kwa kutambua hili, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeunda Taasisi maalum iliyopewa jukumu la kusimamia maadili kwa Viongozi ambayo ni Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar. Kuanzishwa kwa Taasisi hii ni mwendelezo wa jitihada za Serikali katika kuimarisha Utawala Bora Zanzibar. Nchi nyingi duniani zimekuwa mstari wa mbele katika kulinda na kusimamia suala la maadili. Zanzibar ikiwa ni sehemu ya dunia haikuwa nyuma katika kutekeleza jambo hili kupitia Tume ya Maadili.

Baada ya kuanzishwa kwake, Tume ya Maadili imekuwa ikitekeleza kazi zake kama zilivyoainishwa katika Sheria Nam. 4 ya 2015 zikiwemo kupokea, kusajili na kuhakiki Tamko la Mali na Madeni kutoka kwa Viongozi wa Umma, kupokea malalamiko na kufanya uchunguzi kuhusu uvunjaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kutoa elimu kwa umma na viongozi kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili.

copy

Utekelezaji wa kazi hizo umeelezwa katika Ripoti hii kulingana na Mpangokazi wa mwaka wa Tume na Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2016/2017. Aidha, utekelezaji huo wa kazi za Tume umezingatia Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015 pamoja na Mipango Mikuu ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya 2020, MKUZA III na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kipindi cha 2015-2020.

Licha ya upya wa Taasisi hii, Tume inajivunia mafanikio ambayo imeyapata katika kipindi kifupi tangu kuanzishwa kwake kutokana na usimamizi mzuri wa misingi ya uwazi, uadilifu, uwajibikaji, utaalamu

na ushirikiano kutoka Taasisi nyengine katika kutekeleza kazi zake za kila siku.

Ripoti hii imeandaliwa ili kukidhi matakwa ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015 kwa lengo la kubaininisha kazi ambazo zimetekelezwa na Tume.

copy

## 2.0 HISTORIA FUPI YA TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015 ilitayarishwa na Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi tarehe 30 Januari, 2015 na kutiwa saini na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 29 Mei, 2015. Sheria hiyo ilianza kutumika rasmi tarehe 15 Aprili, 2016 baada ya kutangazwa na Waziri wa Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika Tangazo la Kisheria Nam. 34 la mwaka 2016. Aidha, Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho kwa Sheria Nam. 5 ya 2016 na Sheria Nam. 4 ya 2017 ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Tume ya Maadili ni Wakala wa Serikali na imepewa mamlaka na wajibu wa kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Maadili kwa kupokea na kufanya uchunguzi kuhusu malalamiko, tuhuma, madai au taarifa za ukiukwaji wa maadili ya viongozi. Aidha, kupokea, kusajili na kuhakiki Tamko la Mali na Madeni kutoka kwa Viongozi wa Umma pamoja na kutoa elimu kwa viongozi na wananchi kuhusu umuhimu wa maadili.

copy

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alimteua Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Viongozi tarehe 28 Aprili, 2016 na Makamishna wa Tume waliteuliwa tarehe 25 Julai, 2016. Hivyo, Tume inaundwa na wajumbe wafuatao:

1. Mhe. Assaa Ahmad Rashid - Mwenyekiti
2. Mhe. Said Bakari Jecha – Kamishna
3. Mhe. Sebtuu Mohammed Nassor – Kamishna

Maandalizi ya utekelezaji wa kazi za Tume yalianza mwezi wa Aprili, 2016 ikiwa na watumishi wanne (4) walioazimwa kutoka (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.Watumishi wengine waliongezwa kadri ya mahitaji yalivyojitokeza. Hadi kufikia mwezi Juni, 2017 Tume ina jumla ya watumishi wa kudumu 16 baada ya taratibu za uhamisho kukamilika.

Kwa sasa Ofisi Kuu za Tume zinapatikana katika Jengo la zamani la (OR), Kazi na Utumishi wa Umma – Shangani Zanzibar kwa Unguja. Ofisi ya Tume ya Maadili Pemba, ambayo ni kiungo katika kuratibu, kusimamia na kutekeleza kazi zote za Tume ya Maadili ya Viongozi kwa upande wa Pemba, ipo katika jengo la (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar ni miongoni wa Taasisi zinazojitegemea iliyo katika (OR), Katiba, Sheria, utumishi wa Umma na Utawala Bora.

copy

## 2.1 DIRA

Dira ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni *"Kuwa na jamii yenye kufuata maadili"*

## 2.2 DHAMIRA

Dhamira ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni *"Kukuza tabia na vitendo vyenye kufuata maadili kwa viongozi wa umma kwa kuimarisha uwazi, uwajibikaji, utii na usimamizi wa sheria*".

## 2.3 MAADILI YA MSINGI

Utendaji kazi wa Tume ya Maadili umejengwa na unazingatia misingi ya maadili ifuatayo ambayo inawaongoza watumishi wake:

(a) **Uadilifu:** Kufanya kazi kwa uwazi na bila ya upendeleo;

(b) **Usiri:** kuhifadhi na kutunza taarifa zote za siri ikiwemo taarifa zinazohusiana na mali na madeni ya Viongozi wa Umma;

(c) **Utaalamu:** Kusimamia sheria ya Maadili ya Viongozi kwa umakini na uaminifu kwa kutumia umahiri, uweledi, na utaalamu unaohitajika;

(d) **Uwajibikaji:** Kuimarisha uwajibikaji kwa watumishi na wahusika wengine wa Tume; na

(e) **Kufanya kazi kwa mashirikiano:** Kukuza na kuimarisha ushirikiano miongoni mwa watumishi ili kuwezesha utendaji wa kazi za Tume kwa ufanisi.

## 2.4 LENGO KUU

Lengo kuu la Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni *"Kusimamia maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar"*

copy

## 2.5 MUUNDO WA TUME

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume inaundwa na Mwenyekiti (Mtendaji) na Makamishna wawili (wa muda) ambao wanateuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mweyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 10A cha Sheria hiyo, kutakuwa na Katibu wa Tume ambaye anateuliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Katibu wa Tume anakuwa Afisa Mtendaji na kwa nafasi yake anawajibika kwa Tume kwa kazi za kiutawala za kila siku. Aidha, Tume ina watumishi wa fani nyengine tofauti kwa kuzingatia mahitaji yake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

Kwa mujibu wa muundo unaopendekezwa, Tume itakuwa na Idara mbili ambazo ni; Idara ya Mipango, Utawala na Rasilimali Watu na

Idara ya Maadili na Uchunguzi. Pia, Ofisi ya Tume ya Maadili Pemba ndio yenye kuratibu kazi zote za Tume kwa upande wa Pemba.

## 2.6 MAJUKUMU YA TUME

Kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha Sheria ya Maadili, Tume ya Maadili ina majukumu yafuatayo:

(a) Kupokea na kuhifadhi Tamko la Mali na Madeni ambalo limetolewa na Kiongozi wa Umma chini ya Sheria hii;

(b) Kupokea tuhuma na taarifa za uvunjaji wa maadili kutoka kwa wananchi;

(c) Kufanya uchunguzi juu ya madai au tuhuma za uvunjaji wa maadili kwa kiongozi yeyote wa Umma;

copy

(d) Kupokea, kuchunguza na kushughulikia madai yote yanayohusu uvunjaji wa maadili katika chombo cha umma;

(e) Kupokea na kuchunguza jambo lolote ambalo kwa maoni ya Tume linapelekea tuhuma ya moja ya mambo yafuatayo kuwa limetokea au linaweza kutokea:

   (i) Kitendo kinachopelekea uvunjaji wa maadili;

   (ii) Kitendo kinachopelekea kuruhusu, kushawishi au kusababisha uvunjaji wa maadili;

(f) Kuchunguza mwenendo wa kiongozi yeyote wa umma ambao kwa maoni ya Tume, unapelekea au unachangia uvunjaji wa maadili chini ya Sheria hii;

(g) Kusikiliza na kutoa maamuzi kuhusu madai yoyote ya uvunjaji wa Maadili dhidi ya Kiongozi wa Umma;

(h) Kutoa uamuzi wa uvunjaji wowote wa maadili;

(i) Kusaidia taasisi yoyote ya Serikali yenye jukumu la kutekeleza Sheria katika kufanya uchunguzi wa kosa la uvunjaji wa maadili;

(j) Kutokana na maombi ya mtu au taasisi yoyote, kushauri au kusaidia mtu au taasisi yoyote namna ambavyo kiongozi au taasisi hiyo inavyoweza kuepukana na uvunjaji wa maadili;

(k) Kuelimisha umma juu ya umuhimu wa maadili;

(l) Kufanya uchunguzi juu ya jambo lolote ambalo kwa maoni ya Tume linastahili kufanyiwa uchunguzi;

(m) Kutoa ushauri, maelekezo na miongozo kuhusiana na maadili ya viongozi;

(n) Kufanya uhakiki wa moja kwa moja kuhusiana na Tamko la Mali na Madeni lililowasilishwa kwa mujibu wa sheria; na

(o) Kufanya kazi nyengine zozote ilizopewa na Sheria ya Maadili ya Viongozi au Sheria nyenginezo.

copy

## 2.7 MAMLAKA NA UWEZO WA TUME

Katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake, Tume ya Maadili imepewa mamlaka na uwezo wa:

(a) Kumuidhinisha ofisa wa Tume kufanya uchunguzi wa tuhuma ya uvunjaji wa maadili (kif. 13).

(b) Kumtaka mtu yeyote kutoa kumbukumbu na nyaraka zozote zinazohusiana na tuhuma zinazofanyiwa uchunguzi (kif. 13).

(c) Kumtaka mtu yeyote kufika mbele ya Tume kwa ajili ya kuhojiwa kuhusiana na jambo lolote linaloshughulikiwa na Tume katika uchunguzi wa tuhuma za uvunjaji wa maadili (kif.13).

(d) Kumtaka Kiongozi wa Umma kutoa taarifa au maelezo ya ziada kuhusiana na Tamko la Mali na Madeni alililoliwasilisha (kif.16A).

(e) Kushirikiana na taasisi au mtu yeyote katika uchunguzi wa madai au tuhuma za uvunjaji wa Sheria ya Maadili (kif. 14).

(f) Kuchunguza Akaunti ya Kiongozi wa Umma (kif.37).

(g) Kuwasilisha maamuzi yake kwenye mamlaka husika (kif. 27, 3).

## 3.0 KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2016/17

Katika kipindi cha mwaka 2016/2017 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

(a) Uanzishaji wa Ofisi;

(b) Kupokea, kusajili na kuhakiki Taarifa za Mali na Madeni za Viongozi wa Umma;



copy

(c) Kutayarisha mfumo wa ndani wa kielektroniki wa usajili wa taarifa za mali na madeni;

(d) Kupokea na kufanya uchunguzi wa tuhuma na malalamiko ya ukiukaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(e) Kutoa elimu kwa Umma na Viongozi kuhusu umuhimu wa maadili; na

(f) Kutayarisha Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

## 4.0 UTEKELEZAJI HALISI WA KAZI ZA TUME KWA MWAKA 2016/2017

Tume imetekeleza kazi zake kama ifuatavyo:-

### 4.1 UANZISHAJI WA OFISI

copy

Kwa kuwa Tume ni Taasisi mpya, Serikali ilichukua juhudi za kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake kiufanisi kwa kuipatia Ofisi, vitendea kazi na watumishi wanaohitajika.

#### 4.1.1 Ofisi ya Tume

Serikali iliipatia Tume Ofisi ya muda katika jengo la zamani la (OR) Kazi na Utumishi wa Umma pamoja na Watumishi wa kada mbalimbali. Tume ililazimika kuazima baadhi ya Watumishi wenye uzoefu kutoka Wizara na Taasisi tofauti za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika fani za Sheria, Mipango, Utunzaji wa kumbukumbu, Utumishi, Utawala, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Elimu kwa Umma, Ununuzi na Uhasibu. Katika kipindi hiki cha utekelezaji, Tume ina jumla ya watumishi kumi na sita (16), ambapo kati ya hao saba (7) ni wanawake na tisa (9) ni wanaume. Juhudi za kupata Watumishi wengine wenye uzoefu bado zinaendelea kulingana na

mahitaji ya Tume. Idadi ya Watumishi na viwango vyao vya elimu ni kama inavyoonekana katika jadweli **Nambari 1**.

**Jadweli Nambari. 1: Idadi ya Watumishi wa Tume na Viwango vyao vya Elimu.**

| CHETI/ FORM II-VI | | STASHAHADA | | STASHA HADA YA JUU | | SHAHADA | | STASHAH ADA YA UZAMILI | | SHAHADA YA UZAMILI | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | |
| **-** | **2** | **3** | **-** | **-** | **-** | **2** | **3** | **1** | **2** | **1** | **2** | **16** |

### 4.1.2 Upatikanaji wa Samani na Vitendea kazi

Katika kuimarisha mazingira ya utendaji kazi za kila siku, Tume imenunua samani na vitendea kazi vya aina mbalimbali vikiwemo meza, viti, makabati, kompyuta, fotokopi, vifaa vya kuandikia, printa, tajuri kwa ajili ya kuhifadhia Fomu za Matamko ya Mali na Madeni ya Viongozi n.k. Upatikanaji huu wa samani na vitendea kazi mbalimbali umechangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha utekelezaji wa kazi za Tume ilizojipangia kwa urahisi na ufanisi.

copy

### 4.1.3 Kuwajengea Uwezo Watumishi wa Tume

Katika kuwajengea uwezo na hatimaye kuwa na utendaji mzuri wa kazi, Tume imewapatia watumishi wake mafunzo mbalimbali yakiwemo; uelewa juu ya mambo ya msingi yanayohusiana na masuala ya maadili na umuhimu wake, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Utaratibu wa Ujazaji, Upokeaji na Uhifadhi wa Fomu za Tamko la Mali na Madeni, Uhakiki na Uchunguzi. Mafunzo hayo yaliendeshwa na Maofisa Waandamizi kutoka Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tanzania Bara katika Ofisi za Tume ya Maadili Shangani, Unguja. Aidha, mfanyakazi mmoja alihudhuria mafunzo ya muda mfupi ya Uendeshaji wa Ofisi na Utunzaji wa Kumbukumbu

yaliyotolewa na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Kampasi ya Zanzibar. Vilevile, Watendaji watatu walishiriki ziara ya kubadilishana uzoefu na Watendaji wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tanzania Bara mara baada ya kuanzishwa kwa Tume.

### 4.1.4 Muundo wa Kitaasisi wa Tume

Tume iliandaa mapendekezo ya Muundo wa Kitaasisi wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mujibu wa mahitaji na majukumu yake kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa majukumu hayo. Muundo huo wa Tume ya Maadili unaainisha, kuelezea na kugawa majukumu hayo kwa watumishi wake ili kufanikisha utendaji mzuri wa kazi za Tume ya Maadili.

Mapendekezo hayo yalizingatia uzoefu wa taasisi za nchi mbalimbali zinazofanana kimajukumu na Tume ya Maadili. Nchi hizo ni pamoja na Tanzania Bara, Uganda, Ethiopia na Kenya. Muundo huo uliwasilishwa kwa mara ya kwanza katika kikao cha 116 cha Kamisheni ya Utumishi wa Umma kilichofanyika tarehe 28 Disemba, 2016. Kufuatia marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, yaliyopelekea mabadiliko ya muundo wa Tume, mapendekezo hayo yaliwasilishwa tena katika kikao kilichofanyika tarehe 27 Julai, 2017 kwa ajili ya kupitishwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka nyengine za maamuzi kwa kuidhinishwa.

copy

## 4.2 KUPOKEA, KUSAJILI NA KUHAKIKI TAARIFA ZA MALI NA MADENI ZA VIONGOZI WA UMMA

Kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kila kiongozi wa umma anawajibika kujaza na kuwasilisha Tume Fomu ya Tamko la Mali na Madeni. Fomu hiyo ya Tamko

inatakiwa kuwasilishwa kila ifikapo Disemba ya kila mwaka, ndani ya siku thelathini (30) baada ya kushika madaraka au wadhifa wa uongozi na mara tu baada ya kumaliza muda wa kushika madaraka au wadhifa wa uongozi. Viongozi wa Umma, kwa mujibu wa Jadweli ya Kwanza ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, inajumuisha:

(a) Rais wa Zanzibar.
(b) Wateule wote wa Rais wa Zanzibar.
(c) Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.
(d) Wateule wote wa Waziri.
(e) Mahakimu.
(f) Maofisa wa Sekretariet ya Baraza la Mapinduzi.
(g) Madiwani.
(h) Masheha.
(i) Wahasibu wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.
(j) Wakaguzi wa Ndani wa Hesabu wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.
(k) Mganga Mkuu.
(l) Daktari Dhamana.
(m) Muuguzi Mkuu.
(n) Matroni.
(o) Viongozi wengine wenye kushika nafasi kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar au Sheria nyengine yoyote ya Zanzibar.

### 4.2.1 Kupokea na Kuhifadhi Tamko la Mali na Madeni kwa Viongozi wa Umma

Kabla ya kuanza kutoa Fomu za Tamko la Mali na Madeni kwa Viongozi wa Umma, Tume iliziandikia Wizara, Idara na Taasisi za Serikali na kuzitaka kuwasilisha Tume majina na vyeo vya Viongozi wa Umma waliomo katika Wizara, Idara na Taasisi hizo kwa lengo la kuwatambua na kupata taarifa zao za msingi. Baada ya kupatikana


taarifa hizo, Tume iliwaandikia barua viongozi wote wa umma zilizoambatanishwa na Fomu za Tamko la Mali na Madeni ambazo zilitolewa kupitia mikutano mbalimbali iliyofanywa kati ya Tume na viongozi hao.

Fomu hizo pia ziliweza kupatikana katika ofisi za Tume Unguja na Pemba na kwenye tovuti ya Tume ya Maadili. Baada ya kukamilika kazi ya utoaji wa fomu, viongozi hao walipaswa kuzijaza na kuziwasilisha Tume ya Maadili si zaidi ya tarehe 31 Disemba, 2016. Hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2016 jumla ya fomu 1,350 za Viongozi zilipokelewa. Hata hivyo, Tume iliendelea kupokea fomu kutoka kwa viongozi waliochelewa na waliopata uteuzi mpya baada ya tarehe 31 Disemba, 2016. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017 Tume ilipokea jumla ya fomu za Viongozi 1,620, sawa na asilimia 101 ya shabaha iliyopangwa ya Fomu za Tamko la Mali na Madeni 1,600. Kati ya fomu 1,620, viongozi waliowasilisha fomu ndani ya wakati ni 1,479 sawa na asilimia 91 ikijumuisha viongozi 1,350 na 129 hadi kufikia tarehe 31 Juni, 2017. Viongozi waliowasilisha Fomu nje ya wakati ni 141 sawa na aslimia 9. Viongozi wote waliowasilisha fomu walipewa barua za uthibitisho wa kupokelewa fomu zao. Muhtasari wa uwasilishaji Fomu kiasilimia ni kama inavyoonekana katika **Chati Nambari 1**.

copy

Orodha ya waliowasilisha fomu ilichapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali (Tangazo la Kisheria Nambari 10 na 40 la mwaka 2017), kama kifungu cha 22(3) cha Sheria ya Maadili kinavyoelekeza.

**Chati Nambari 1.**




### 4.2.2 Kuhakiki Taarifa za Mali na Madeni za Viongozi wa Umma


Tume ya Maadili baada ya kupokea Fomu za Matamko ya Mali na Madeni ya yaliyojazwa na kurejeshwa, ilifanya kazi ya usajili na kuyaweka katika Daftari la Usajili. Ili kuhakikisha usahihi wa matamko hayo, Tume kwa mujibu wa kifungu cha 12.-(1)(n), katika awamu ya kwanza ilihakiki taarifa za baadhi ya Viongozi wa Umma kwa kushirikiana na wataalam (Wathamini) kutoka Kamisheni ya Ardhi Zanzibar na Shirika la Nyumba Zanzibar. Kazi ya msingi waliyoifanya Wataalamu hao ni kuhakiki thamani za mali zilizotajwa katika Fomu za Tamko kwa kuzingatia thamani halisi ya wakati wa ujenzi au ununuzi pamoja na thamani ya sasa ya soko.

copy

Kazi ya uhakiki ilianza rasmi Tarehe 5 Juni, 2017 ambapo shabaha ya Tume kwa kuanzia ilikuwa ni kukagua Viongozi 56 kwa mwaka 2016/2017. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017 jumla ya viongozi thelathini na nane (38) walifanyiwa uhakiki wa taarifa zao kwa upande wa Unguja. Hii ni sawa na asilimia 68 ya waliopangiwa

kuhakikiwa kwa mwaka 2016/2017. Muhtasari wa uhakiki kiasilimia ni kama unavyoonekana katika chati Nambari. 2.

**Chati Nambari 2:**




copy

Aidha, kwa upande wa baadhi ya viongozi ambao mali zao ziko Pemba na Tanzania Bara, Tume imepanga kuzihakiki mali hizo katika robo mwaka ya kwanza (Julai-Septemba, 2017) ya mwaka wa fedha 2017/2018 na hivyo kukamilisha idadi ya awamu ya kwanza ya kazi ya uhakiki wa taarifa za mali na madeni kwa (56).

## 4.3 KUTAYARISHA MFUMO WA NDANI WA KIELEKTRONIKI WA USAJILI WA TAARIFA ZA MALI NA MADENI

Tume imeandaa Mfumo wa Ndani wa Ki-elektroniki kwa ajili ya kusajili taarifa za . Kazi hii ya kutayarisha mfumo wa ndani wa ki-elektroniki bado inaendelea ambapo katika hatua za awali taarifa za msingi za viongozi wote wa umma zimeingizwa. Matarajio ya Tume ni kwamba mfumo huu mara tu utakapokamilika utarahisisha uhifadhi na upatikanaji wa taarifa na pia kupunguza gharama nyengine za

uendeshaji. Shughuli hii inatekelezwa kwa msaada wa kitaalam kutoka Idara ya Serikali Mtandao (e-Government).

## 4.4 KUPOKEA NA KUFANYA UCHUNGUZI WA TUHUMA NA MALALAMIKO YA UKIUKAJI WA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Kwa mujibu wa kifungu cha 12.-(1)(a)-(d) cha Sheria ya Maadili, Tume imepewa mamlaka na wajibu wa kupokea na kufanya uchunguzi kuhusu malalamiko, tuhuma, madai au taarifa za ukiukwaji wa maadili ya viongozi.

### 4.4.1 Tuhuma na Malalamiko

Katika kipindi hiki cha utekelezaji, Tume imepokea na kufanyia kazi malalamiko manne (4) kutoka kwa wananchi yanayohusiana na uvunjaji wa Sheria ya Maadili kwa Viongozi wa Umma. Mashauri hayo bado yanaendelea kufanyiwa uchunguzi na yatakapokamilika Tume itawasilisha maamuzi yake kwa mamlaka zinazohusika. Aina za Tuhuma pamoja na idadi yake ni kama zinavyoonekana katika **jadweli Nambari 2**.

copy

**Jadweli Nambari 2: Idadi ya Malalamiko/Tuhuma/Taarifa**

| NAM. | MALALAMIKO/TUHUMA/TAARIFA | IDADI | HATUA | HALI HALISI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Matumizi mabaya ya madaraka | 3 | Maelezo yamechukuliwa<br><br>Vielelezo vimekusanywa | Uchunguzi unaendelea |
| 2. | Udhalilishaji wa kijinsia | 1 | Maelezo yamechukuliwa | Uchunguzi unaendelea |

### 4.4.2 Uvunjaji wa Maadili

Viongozi ambao hawakuwasilisha kabisa au walichelewa kuwasilisha fomu zao waliandikiwa barua za kujieleza na kutakiwa kutoa sababu za kushindwa kuwasilisha fomu kwa wakati au kutowasilisha kabisa. Jumla ya Viongozi 6 hawakuwasilisha fomu na viongozi 141 walichelewa kuwasilisha fomu zao. Viongozi hao walipewa barua za taarifa ya kuchelewa kuwasilisha Fomu. Miongoni mwa viongozi hao walitakiwa kutoa maelezo kwa maandishi kuhusu sababu za kushindwa kwao kuwasilisha fomu kwa wakati uliowekwa kisheria au kushindwa kuwasilisha kabisa. Baadhi ya viongozi hao tayari wameshaitwa mbele ya Tume ya Maadili kwa ajili ya kujieleza zaidi na kutoa ufafanuzi juu ya utetezi wao.

Tume imeendelea kuyafanyia kazi mashauri ya walioshindwa kuwasilisha Fomu za Tamko la Mali na Madeni kwa wakati (tarehe 31 Disemba, 2016) na walioshindwa kabisa kujaza na kuwasilisha fomu hizo, kama inavyoonekana katika **Jadweli Nambari 3 na 4**.

copy

**Jadweli Nambari 3: Waliochelewa kuwasilisha Fomu.**

| NAM. | MAELEZO | IDADI | HATUA | HALI HALISI |
|---|---|---|---|---|
| | | **Waliochelewa** | | |
| 1. | Waliochelewa kuwasilisha fomu kwa wakati | 141 | Barua za taarifa ya kuchelewa zilitolewa kwa Viongozi wote | Viongozi wameandikiwa barua za kutoa sababu za kuchelewa |
| | Uteuzi wa Rais | 12 | Barua kutoa sababu za kuchelewa zilitolewa<br><br>Maelezo ya utetezi yamewasilishwa | Hatua na taratibu za Kisheria zinaendelea |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Uteuzi wa Waziri | 13 | Barua kutoa sababu za kuchelewa zilitolewa | Hatua na taratibu za Kisheria zinaendelea |
| | Viongozi Wengine | 116 | Barua kutoa sababu za kuchelewa zilitolewa | Fomu za Masheha na Madiwani zilichelewa kuwasilishwa Tume kutoka Ofisi za Wilaya |
| 2. | Walioitwa mbele ya Tume | 2 | Mashauri yalisikilizwa | Hatua na taratibu za Kisheria zinaendelea |

**Jadweli Nambari 4: Walioshindwa Kuwasilisha Fomu**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Wasiowasilisha fomu | 6 | Barua za kujieleza zilitolewa<br><br>Maelezo ya utetezi yamewasilishwa | Viongozi wawili (2) walikuwa katika masomo ya muda mrefu na mmoja mgonjwa. |
| 2. | Walioitwa mbele ya Tume | 2 | Mashauri yalisikilizwa | Hatua na taratibu za Kisheria zinaendelea |

copy

## 4.5 KUTOA ELIMU KWA UMMA NA VIONGOZI KUHUSU UMUHIMU WA MAADILI

Utoaji wa elimu ya Maadili ni miongoni mwa majukumu ya msingi ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 12.-(1)(k) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Zifuatazo ni njia mbalimbali za utaoji wa elimu kwa umma na ambazo Tume imezitumia katika kipindi hiki cha utekelezaji:-

### 4. 5.1 Mikutano ya Viongozi wa Umma

Tume ilitoa elimu kwa Viongozi mbalimbali wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia mikutano. Mikutano hiyo ilijumuisha Watendaji Wakuu wa Wizara, Idara, Mashirika na Taasisi za Umma ambao kwa mujibu wa Sheria ya Maadili wanawajibika kujaza Fomu ya Tamko la Mali na Madeni.

Jumla ya Mikutano 30 ilifanyika kati ya hiyo Unguja 24 na Pemba 6 (Kama inavyoonekana katika **kiambatanisho Nam. 1**). Mada kuu zilizowasilishwa kupitia mikutano hiyo ni:

a) Umuhimu wa Maadili kwa Viongozi na Watumishi wa Umma;
b) Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma; na
c) Utaratibu wa kujaza Fomu ya Tamko la Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma.

copy

Kupitia mikutano hiyo, Viongozi wa Umma walipata fursa ya kuuliza masuali mbalimbali kutokana na mada hizo zilizowasilishwa na hatimaye kupatiwa ufafanuzi na maelezo ya kina kutoka kwa Watendaji wa Tume.

### 4.5.2 Utayarishaji na Urushaji wa Vipindi vya Elimu na Matangazo kupitia Vyombo vya Habari

Vyombo vya habari vina mchango mkubwa katika kufikisha elimu kwa jamii, katika kulitambua hilo Tume haikuwa nyuma katika kuhakikisha kuwa elimu inayohusiana na maadili inawafikia wananchi wote.

Katika kipindi hiki cha utekelezaji, Tume ilitayarisha na kurusha hewani jumla ya vipindi saba (7) kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC). Kati ya hivyo, vipindi vitatu (3) kupitia ZBC

Televisheni na vipindi vinne (4) kupitia ZBC redio. Vipindi hivyo viliitambulisha Tume kwa Viongozi wa Umma na Wananchi na vilivyozungumzia majukumu, uwezo wa Tume pamoja na wajibu wa Kiongozi wa Umma. Aidha, makala na habari mbalimbali ziliandaliwa na kuchapishwa kupitia Gazeti la Zanzibar Leo pamoja na Magazeti mengine ya Tanzania Bara.

### 4.5.3 Utoaji wa Vipeperushi, Machapisho na Matangazo

Tume iliandaa na kuchapisha jumla ya vipeperushi vya aina mbili (2) 4,500 vyenye maudhui tofauti. Vipeperushi hivyo ni; "IFAHAMU TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA" na "WAJIBU WA KIONGOZI WA UMMA". Ili kuhakikisha ujumbe unawafikia na wananchi, Tume ilisambaza vipeperushi hivyo katika mikutano yote na Viongozi wa Umma na Siku ya kilele cha Maadhimisho ya Maadili na Haki za Binaadamu tarehe 10 Disemba, 2016. Vipeperushi hivyo vilitolewa kwa Viongozi wa Umma na Wananchi waliofika katika sherehe hizo zilizofanyika katika viwanja vya 'Victoria Garden', Zanzibar.

Kwa upande wa Machapisho, Tume ilitoa jumla ya nakala 1,000 za Sheria Nam. 4 ya 2015 ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Fomu 2,627 za Tamko la Mali na Madeni, Fomu 1,000 za malalamiko na Orodha ya Majina ya Viongozi wa Umma waliowasilisha Fomu yaliyochapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Aidha, matangazo mbalimbali kupitia vyombo vya habari yaliandaliwa na kutolewa kwa lengo la kuwakumbusha na wananchi juu ya suala zima la kusimamia maadili katika nchi yetu. Katika kufanikisha hili, wasanii wa vikundi vya utamaduni walitumika ili kufikisha ujumbe kwa wahusika.

copy

### 4.5.4 Tovuti ya Tume

Tume ya Maadili imeendelea kuiimarisha tovuti yake kwa kuingiza taarifa mbalimbali ili kuwawezesha na wananchi kupata taarifa muhimu zinazohusiana na utendaji kazi wa Tume. Kupitia kitengo chake cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, matukio, nyaraka, matangazo na taarifa tofauti zimewekwa katika tovuti ya Tume na kufanya kuwa kituo kikuu cha kutoa habari kwa umma. Ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya kutoa taarifa, Tume inakusudia kuwa na mawasiliano ya mitandao ya kijamii ili kuwa karibu zaidi na jamii. Anuani rasmi ya tovuti hiyo ni *www.ethicscommission.go.tz*. Miongoni mwa taarifa zinazopatikana katika tovuti ya Tume ni kama zifutazo:

(a) Sheria ya Maadili ya Viongozi;
(b) Fomu ya Tamko la Mali na Madeni;
(c) Fomu ya Malalamiko;
(d) Orodha ya Majina ya Viongozi waliowasilisha Fomu ya Tamko la Mali na Madeni;
(e) Vipeperushi; na
(f) Taarifa mbalimbali zinazohusiana na Tume.

copy

### 4.5.5 Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binaadamu

Tume ya Maadili kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, Idara ya Utawala Bora, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Zanzibar iliandaa na kufanikisha kwa pamoja Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binaadamu tarehe 10 Disemba, 2016. Watendaji wa Taasisi hizo walishirikiana katika kuandaa programu mbalimbali ili kufanikisha sherehe hizo zikiwemo; kongamano la Wanavyuo, vipindi vya redio na televisheni, makala na matangazo. Mgeni rasmi katika Maadhimisho hayo ya siku ya Maadili

na Haki za Binaadamu alikuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein.

Sherehe hizo huadhimishwa kila mwaka duniani ambapo kwa Zanzibar ilikuwa ni mara ya kwanza kufanyika kitaifa. Hivyo, kupitia maadhimisho hayo, ilikuwa ni fursa ya kipekee kwa Tume kujitangaza na kuongeza ufahamu kwa na Wananchi juu ya dhana na umuhimu wa maadili. Viongozi, Watendaji, Watumishi wa Umma kutoka Taasisi za Serikali, Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya ndani na nje ya nchi pamoja na Wananchi walialikwa katika sherehe hizo zilizofanyika katika viwanja vya 'Victoria Garden'.

## 4.6 KUTAYARISHA KANUNI ZA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Kazi ya kutayarisha Kanuni za Utekelezaji wa Sheria ya Maadili ya bado haijakamilika. Kazi hii kwa sasa iko katika hatua za mwisho kukamilika na hatimaye kuchapishwa. Kazi hii ilishindikana kukamilishwa kwa wakati ili kusubiri marekebisho ya Sheria ya Maadili baada ya kubainika kwamba baadhi ya vifungu vya Sheria hiyo havijitoshelezi na kupelekea ugumu katika utekelezaji wake. Tume inapongeza kwa kufanyika kwa baadhi ya marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015 kwa lengo la kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

copy

## 5.0 VIKAO VYA TUME

Kama ilivyoelezwa awali katika sehemu ya muundo, Tume inaundwa na Mwenyekiti na Makamishna wawili ambapo hukutana na kufanya maamuzi kupitia vikao vya Tume. Kupitia vikao hivyo malalamiko, madai na taarifa za uvunjaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma husikilizwa na kutolewa maamuzi. Katika kipindi hiki cha

utekelezaji, jumla ya vikao vinne (4) vimefanyika. Vikao hivyo pamoja na mambo mengine vilihusisha upokeaji na upitishaji wa mipango na taarifa mbalimbali za utekelezaji wa kazi za Tume pamoja na kusikiliza na kutoa uamuzi kuhusu malalamiko, madai na taarifa za uvunjaji wa maadili ya .

## 6.0 HALI YA UPATIKANAJI WA FEDHA

Baada ya Tume kuanzishwa rasmi mwezi Aprili, 2016 kiasi cha Shilingi 115,000,000 zilitengwa kupitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya kuanzisha ofisi. Hadi kufikia mwezi Juni, 2016 fedha zilizopatikana ni shilingi 52,737,112 (46%) ambazo zilitumika kwa kununulia samani, vitendea kazi na huduma mbalimbali za Ofisi.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Tume iliidhinishiwa jumla ya Tshs. 120,000,000 kwa matumizi ya kawaida ambapo hadi kufikia mwezi Juni, 2017 fedha zilizopatikana ni Tshs. 117,500,000 sawa na asilimia 98.

## 7.0 CHANGAMOTO NA UTATUZI WAKE

Mbali na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa kazi, Tume inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Zifuatazo ni baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa kazi na njia zilizotumika kutatua baadhi ya changamoto hizo:-

i. Uelewa mdogo kwa Viongozi wa Umma na Wananchi juu ya majukumu na utendaji kazi wa Tume; - Juhudi za kutoa elimu kupitia njia mbalimbali zinaendelea kufanyika kupitia kitengo cha elimu kwa umma.
ii. Kutokukamilika kwa mfumo wa ndani wa kielektroniki wa kuweka na kuhifadhi taarifa za ; - Wataalamu kutoka Idara ya Serikali Mtandao wanaendelea na kazi ya kuukamilisha mfumo

huo kwa kushirikiana na Wataalam wa Tume kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

iii. Viongozi wengi kutokuwa na hati za umiliki wa mali zao kama vile viwanja, mashamba, nyumba na gari; - Tume inashauri kuwa Viongozi wahakikishe wanakamilisha taratibu za uhaulishaji au upatikanaji wa hati za umiliki wa mali zao kisheria.

iv. Fomu nyingi za Matamko ya Mali na Madeni zilizowasilishwa Tume zimeonekana kuwa na upungufu katika baadhi ya sehemu katika ujazaji pamoja na kukosa baadhi ya vielelezo; - Elimu kuhusiana na ujazaji wa fomu kikamilifu imeendelea kutolewa kupitia mikutano na semina mbalimbali za Viongozi wa Umma, program za utoaji wa elimu na kwa viongozi wanaofika ofisi za Tume.

v. Viongozi wengi wa Umma walirejesha Fomu za Tamko la Mali na Madeni tarehe za mwisho kabla muda uliowekwa kisheria na kupelekea usumbufu kwa viongozi wenyewe na watendaji wa Tume; - Tume inashauri Fomu zianze kuwasilishwa wiki ya mwanzo ya mwezi wa Disemba kila mwaka.

copy

vi. Ukosefu wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi za Tume; - Tume iliazima vyombo vya usafiri kufanikisha kazi zake.

## 8.0 MIKAKATI YA TUME KWA MWAKA 2017/2018

Tume imepanga kutekeleza kwa mwaka wa fedha 2017/2018 mikakati ifuatayo:-

i. Kukamilisha mfumo wa ndani wa ki-elektroniki utakaotumika katika kusajili na kuhifadhi taarifa za mali na madeni;

ii. Kuendelea na kazi ya uhakiki wa taarifa za mali na madeni za Viongozi wa Umma;

iii. Kuongeza kasi ya uchunguzi wa tuhuma za ukiukaji wa Sheria ya maadili ya viongozi;

iv. Kutumia njia na mbinu mbalimbali za kujenga uelewa kwa wananchi na Viongozi wa Umma  Unguja na Pemba kuhusu umuhimu wa Maadili ya Viongozi; na

v. Kuwajengea uwezo Watumishi wa Tume katika eneo la Uongozi na Maadili, Usajili, Uhakiki, Uchunguzi, nk.

## 9.0 MAPENDEKEZO

Ili kufanikisha utekelezaji wa kazi zake, Tume inapendekeza mambo yafuatayo:-

i. Kupatiwa gari kwa ajili ya ufuatiliaji na utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Tume;

ii. Mamlaka husika ziwashajiishe Viongozi na Wananchi kwa ujumla juu ya umuhimu wa kuwa na hati za umiliki wa mali zao kama vile za viwanja, mashamba, nyumba na gari; na

iii. Kuwepo kwa Muundo wa Kitaasisi wa Tume ya Maadili kutasaidia kubainisha, kuelezea na kugawa majukumu ya Tume kwa watendaji wake na kufanikisha utendaji mzuri wa kazi za Tume.

copy

## 10.0 HITIMISHO

Kazi ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar ya kuhakikisha inasimamia maadili imekuwa na mafanikio. Kupokea, kusajili na kuhakiki Tamko la Mali na Madeni kutoka kwa Viongozi wa Umma, kufanya uchunguzi kuhusu uvunjwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kutoa Elimu kwa umma na viongozi kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili ni miongoni mwa kazi za msingi zilizofanyika katika kipindi hiki cha utekelezaji kwa mwaka 2016/2017.

Ni ukweli usiopingika kuwa suala la maadili si la Viongozi wa Umma tu na wale wote waliotajwa katika Sheria bali ni la wananchi wote. Pamoja na upya wa taasisi, baadhi ya changamoto mbalimbali zilizojitokeza ziliweza kutatuliwa kwa njia moja au nyengine. Tume ina imani kuwa kadri siku zinavyokwenda viongozi pamoja na jamii kwa ujumla wataweza kuuzoea utaratibu huu mpya.

Ushirikiano mkubwa ilioupata Tume kutoka Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Viongozi na Wananchi kwa ujumla, umechangia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Tume katika kipindi hiki cha utekelezaji. Bila ya ushirikiano huo, Tume isingeweza kutekeleza kazi zake kwa ufanisi. Kwa mnasaba huo, wito unatolewa kwa Viongozi na Wananchi kwa ujumla kuendelea kuipa ushirikiano Tume ili lengo kuu la Serikali la kuwaletea wananchi maendeleo na ustawi wa jamii lifanikiwe kikamilifu.

copy

Kadhalika, juhudi za utoaji elimu zitapewa kipaumbele katika mipango ijayo ya Tume kwa lengo la kuhakikisha Viongozi wa Umma pamoja na Wananchi wana uelewa wa kutosha kuhusiana na umuhimu wa maadili.

Ni matumaini ya Tume kuwa Ripoti hii ya kwanza ya Tume ya Maadili itatoa mwanga wa kutosha kuhusu majukumu ya Tume, wajibu wa Viongozi wa Umma na wananchi na kazi za Tume zilizotekelezwa katika kipindi hiki.

## 11.0 UWASILISHAJI WA RIPOTI

Ripoti hii inawasilishwa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa kifungu cha 29(1) na (2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015, leo tarehe 29 Septemba, 2017.

**Naomba kuwasilisha.**

**ASSAA A. RASHID**
**MWENYEKITI**
**TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**
**ZANZIBAR.**

copy

| **Kiambatanisho Nambari 1: RATIBA YA MIKUTANO YA VIONGOZI WA UMMA** | | |
|---|---|---|
| **MIKUTANO-PEMBA** | | |
| **TAREHE YA KIKAO** | **WASHIRIKI** | **MAHALI/UKUMBI** |
| 16 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | MASHEHA NA MADIWANI WA WILAYA YA CHAKECHAKE | OFISI YA MKUU WA WILAYA YA CHAKECHAKE |
| 16 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | MASHEHA NA MADIWANI WA WILAYA YA MKOANI | OFISI YA MKUU WA WILAYA YA MKOANI |
| 17 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | MASHEHA NA MADIWANI WA WILAYA YA MICHEWENI | OFISI YA MKUU WA WILAYA YA MICHEWENI |
| 17 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | MASHEHA NA MADIWANI WA WILAYA YA WETE | OFISI YA MKUU WA WILAYA YA WETE |
| 18 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | WAHASIBU, WAKAGUZI WA NDANI WA WIZARA, IDARA NA TAASISI ZA SERIKALI; WAHASIBU NA WAKAGUZI WA MIKOA, WILAYA, MABARAZA NA HALMASHAURI. | GOMBANI |
| 22 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | WAKUU WA MIKOA , WAKUU WA WILAYA , KATIBU TAWALA WA MIKOA NA WILAYA, MAAFISA WADHAMINI NA IDARA/TAASISI, MAHAKIMU, WASHAURI WA RAIS, WAKURUGENZI WA HALMASHAURI NA MABARAZA | ZSTC - MAKONYO |
| **MIKUTANO-UNGUJA** | | |
| **TAREHE YA KIKAO** | **WASHIRIKI** | **MAHALI/UKUMBI** |
| 16 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | BARAZA LA MAPINDUZI | IKULU |
| 22 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI | WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI |

COPY

| | | |
|---|---|---|
| 22 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE, VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO | WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE, VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO |
| 23 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | WAKUU WA MIKOA, WAKUU WA WILAYA, KATIBU TAWALA WA MIKOA NA WILAYA, WAKURUGENZI WA HALMASHAURI NA MABARAZA, WAHASIBU NA WAKAGUZI. | OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI |
| 23 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI | WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI |
| 24 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI | UKUMBI MDOGO JUMBA LA WANANCHI |
| 24 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | WIZARA YA ARDHI, MAJI NISHATI NA MAZINGIRA | WIZARA YA ARDHI, MAJI NISHATI NA MAZINGIRA |
| 26 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | BARAZA LA WAWAKILISHI | BARAZA LA WAWAKILISHI |
| 28 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | (OR) KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA | OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI |
| 28 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | WIZARA YA AFYA | WIZARA YA AFYA |
| 29 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS | OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS |
| 29 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | (OR) TAWALA ZA MIKOA ZA MIKOA NA IDARA MAALUM ZA SMZ | (OR) TAWALA ZA MIKOA ZA MIKOA NA IDARA MAALUM ZA SMZ |
| 30 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | MAHKAMA | OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI |
| 30 NOVEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRI | WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI |

copy

| | | |
|---|---|---|
| 1 DISEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO (ZRB, PBZ, ZSSF, MFUKO WA BARABARA, BIMA). | WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO |
| 1 DISEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO | WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO |
| 5 DISEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO | WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO |
| 5 DISEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | MASHEHA NA MADIWANI WA WILAYA YA MJINI | OFISI YA MKUU WA WILAYA YA MJINI |
| 6 DISEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | MASHEHA NA MADIWANI WA WILAYA YA MAGHRIB "A" | OFISI YA MKUU WA WILAYA YA MAGHRIBI "A" |
| 6 DISEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | MASHEHA NA MADIWANI WA WILAYA YA MAGHRIB "B" | OFISI YA MKUU WA WILAYA YA MAGHRIBI "B" |
| 7 DISEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | MASHEHA NA MADIWANI WA WILAYA YA KASKAZINI "A" + TUMBATU | OFISI YA MKUU WA WILAYA YA KASKAZINI "A" |
| 7 DISEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | MASHEHA NA MADIWANI WA WILAYA YA KASKAZINI "B" | OFISI YA MKUU WA WILAYA YA KASKAZINI "B" |
| 8 DISEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | MASHEHA NA MADIWANI WA WILAYA YA KUSINI | OFISI YA MKUU WA WILAYA YA KUSINI |
| 8 DISEMBA, 2016 (SAA 3:00 ASUBUHI) | MASHEHA NA MADIWANI WA WILAYA YA KATI | OFISI YA MKUU WA WILAYA YA KATI |

copy